# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

### FOMU YA UHAKIKI WA NYIMBO

**Taarifa za wimbo**

1. **Jina la msanii/kikundi**: Rostam (Roma ft Stamina)
2. **Jina la wimbo**: Abdul
3. **Jina la Mtozi**: Kitunzo
4. **Tarehe ya Kutoka: 26-08-2025**

**Daraja la wimbo**

| WW(U) | WM13(U13) | WM16(U16) | WZ18 (A) | MM (SS) | KK (R) | X |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ✓ | |

**Moani ya Mhakiki**

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limefanya uhakiki wa wimbo *“Abdul”* wa Rostam (Roma Mkatoliki ft. Stamina) uliotolewa tarehe 26 Agosti 2025. Uhakiki umebaini ukiukwaji wa Kanuni za Maadili kwa kutumia lugha ya kudhalilisha na maneno ya uchochezi dhidi ya viongozi wa nchi, kinyume na Kanuni ya BASATA kifungu cha 25(6). Baadhi ya Maneno yenye uchochezi, kebehi na udhalilishaji kwa viongozi wa nchi yaliyotumika ni Pamoja na : “unalinda komwe unaacha tako”, “Hii ni nchi siyo familia, hii Jamhuri babu”, “Siyo falme za Kiarabu”, “Ikulu mnaifanya ka Gheto”, “ila Mama utaniwia radhi halikutoshi hilo vazi” na “Warithi nini na bandari Umempa Mwarabu”.

Kwa kuzingatia matokeo ya uhakiki, wimbo huu umepewa **Daraja KK sawa na R**, hivyo **umepigwa marufuku kuchezwa, kusambazwa au kutumika katika jukwaa lolote** hadi mashairi husika yatakapofanyiwa marekebisho.

BASATA inawakumbusha wasanii wote kuzingatia maadili, heshima na maslahi ya Taifa wanapoandaa kazi zao za sanaa.

**ANGALIZO:**

Vyombo vya Habari vinaaswa kutokucheza wimbo huu wala kuwa na matumizi yoyote na wimbo.

**TAREHE26/08/2025**

**KAIMU MKURUGENZI MSAIDIZI, MUZIKI.**

Jengo la Utumishi, 8 Barabara ya Kivukoni, S. L. P 4779, Dar es Salaam, TANZANIA, Simu: +255 738 259 611/481,

Barua Pepe: km@basata.go.tz / info@basata.go.tz, Tovuti: www.basata.go.tz